BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Thalathini – Tarehe 21 Juni, 2023
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Shilingi Trilioni Mbili, Bilioni Mia Nane na Arobaini, Milioni Mia Nane na Hamsini na Tatu, Laki Saba na Thelathini na Mbili Elfu Kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha Unaoishia siku ya tarehe thelathini Juni, Mwaka wa Elfu Mbili na Ishirini na Nne na kuruhusu utoaji na uhaulishaji wa fedha hizo pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi Zinazohusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Umma na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi Zinazohusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Umma na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

194. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Pamoja na jitihada za Serikali katika kuhakikisha suala la ajira linakaa sawa sambamba na mahitaji ya vijana, bado kuna haja ya Serikali kutoa kipaumbele kinachostahili na kutumia vyema ushauri wa kitaalamu juu ya suala hili.

(a) Je, Serikali inashirikiana vipi na nchi marafiki na Zanzibar katika kuwapatia nafasi Wazanzibari, hasa vijana, katika nchi za nje.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwa na sera bora inayoshughulika na changamoto za watu wanaotafuta ajira za nje.

(c) Kwa kuwa ubaguzi katika ajira umeshamiri na sio sera ya Serikali, Je, Serikali inatumia utaratibu upi kuimarisha upatikanaji wa haki sawa katika ajira bila ya kujali ukabila, rangi, mafungamano ya kisiasa au mahusiano na viongozi wa ngazi za juu.

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

176. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi): Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kuna taarifa kuwa hivi karibuni Serikali ilifanya tafiti na ufuatiliaji wa taasisi zisizo za Serikali (NGOs) zinazofanyakazi hapa Zanzibar.

(a) Je, ukweli wa taarifa hiyo ukoje.

(b) Je, Serikali ilikuwa na lengo lipi la kuifanya kazi hiyo.

### Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

185. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa kuwa uchumi wa Zanzibar unaendelea kuimarika Je, ni lini ahadi za ununuzi wa meli mpya ya abiria itatekelezwa.

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

138. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kuanzishwa Mfuko wa kuwawezesha vijana kwenye kilimo ni jambo jema lenye mafanikio makubwa kiuchumi na ukombozi kwa vijana, endapo Serikali italitilia mkazo na kulipa umuhimu wa kipekee jambo hili.

(a) Je, ni lini Serikali itaanzisha Mfuko huu wa Kilimo kwa Vijana, ili waingie zaidi katika kilimo na kujikomboa na umasikini.

(b) Je, kwa kiasi gani Wizara yako itawapatia vijana hao mafunzo elekezi ya kilimo, ili baada ya kuanzishwa kwa Mfuko huo waweze zaidi kuimarika katika kilimo cha aina mbali mbali hususan cha mboga mboga na matunda.

160. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Katika kuwawezesha vijana wetu kujitegemea, Serikali imefungua milango ya kilimo na kuwapa fursa vijana hao katika kukitegemea kilimo ili kuyaendesha maisha yao.

Je, Serikali ina mkakati upi wa kuwawezesha vijana wetu hususan wahitimu katika vyuo mbali mbali hapa Zanzibar, kunufaika na fursa adhimu za mashamba yaliyopo Tanzania bara.

Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi:

205. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Kuwepo kwa Mahkama za Ardhi kwa nchi ndogo kama Zanzibar, kulitarajiwa kumalizika kwa haki kesi zote za migogoro ya ardhi zilizopo nchini. Hata hivyo, kutokamilika kwa usajili wa ardhi yote kumesababisha kuzorota kwa kazi za Mahkama za Ardhi Zanzibar.

(a) Je, ni ipi ratiba na gharama ya kukamilisha taratibu za kuitambua ardhi yote, kuisajili, kuimilikisha na kuihaulisha kwa wananchi husika kwa taratibu bora.

(b) Je, ni ipi ratiba ya kumaliza kesi zote za migogoro ya ardhi zilizopo na kwa haki.

(c) Kwa kuwa kumekuwa na mkanganyiko katika usimamizi wa ardhi kimamlaka, ni ipi mamlaka sahihi ambayo suala la usimamizi wa ardhi linatakiwa kuanzia.

## Wizara ya Afya:

140. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Tunaipongeza Serikali kwa kujenga hospitali moja kila wilaya kwa ajili ya kuwaondolea changamoto za matibabu wananchi wake.

(a) Je, kwa nini majengo hayo hayana maeneo maalum ya kusubiria wananchi wanaouguza na wale wanaokuja kupata huduma na kuangalia wagonjwa.

(b) Je, hatuoni kuwa kutokuwepo kwa eneo maalum la watu kukaa kunaweza kupekea kukaa sehemu zisizo stahili na kusababisha msongamano ndani ya hospitali hizo.

144. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kumekuwa na malalamiko mengi ya wajasiriamali wanaotaka kuanzisha biashara ya maduka ya madawa kutokana na kikwazo cha fidia ya wadhamini wa maduka hayo, wakilalamikia kuwa ni kubwa mno.

Je, Wizara yako inatoa tamko gani juu ya malalamiko haya.

## Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

225. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Kwa lengo la kuimarisha uchumi, kuinua kipato, pamoja na ustawi wa hali za wananchi wa hali zote, ipo haja kwa Serikali kupitia na kutathmini mikataba ya uwekezaji katika sekta ya mazao ya biashara kama vile mwani na miwa kwa sababu hali ya sasa inanung’unikiwa.

(a) Je, Serikali inasimamiaje haki na maslahi ya wakulima na wawekezaji katika mazao ya biashara kama vile mwani na miwa.

(b) Je, ni ipi takwimu halisi za uendeshaji, uzalishaji, uuzaji, pamoja na mapato yanayotokana na mazao yetu ya biashara (karafuu, mwani, miwa, na viungo) kwa kipindi cha mwaka 2020-2023.

(c) Je, ni kwa kiasi gani mazao makuu ya biashara Zanzibar (karafuu, mwani, miwa, na viungo) yamesaidia katika kukuza uchumi.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

183. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Je, Wizara inafanya tafiti zipi kujua mchango wa Vyuo vya Mafunzo ya Amali Zanzibar.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Shilingi Trilioni Mbili, Bilioni Mia Nane na Arobaini, Milioni Mia Nane na Hamsini na Tatu, Laki Saba na Thelathini na Mbili Elfu Kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha Unaoishia siku ya tarehe thelathini Juni, Mwaka wa Elfu Mbili na Ishirini na Nne na kuruhusu utoaji na uhaulishaji wa fedha hizo pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo – Kusomwa kwa mara ya Pili.

Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi Zinazohusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Umma na mambo mengine yanayohusiana na hayo - Kusomwa kwa mara ya Pili.

Zanzibar,
21 Juni, 2023.

(Abdalla Ali Shauri)
Kny. KATIBU WA BARAZA